

SEKTA YA KILIMO:

Sera na sheria ya Taifa ya Kilimo na Mifugo

Sera ya kilimo na mifugo ya mwaka 1997 ina eleza kwamba:

- Uhuru wa soko na uondoaji wa serikali kuhodhi uingizaji na uuzaji wan je ya nchi wa mazao ya kilimo.
- Tafsiri ya wazi ya kanuni za serikali na sekta binafsi katika uzalishaji na utoaji wa huduma.
- Uwajibikajiwa serikali katika kurekebisha viwanda kupitia bodi ya mazao na
- Usisitizaji wa usalama wa chakula katika ngazi ya taifa na kaya kinyume na kujitosheleza kwa chakula.
- Sheria zinazoiongoza Idara ni:
 - “The Mbinga District Council (Compulsory Cultivation of Crops) by law 1991”
 - “The Mbinga District Council (Crop cess) by law 2000”

Mabadiliko na matukio makuu katika mfumo wa Siasa, Ulinzi, Utawala, Kiuchumi, Kiteknolojia na Kijamii:

Hakukuwa na matukio makuu katika mfumo wa Siasa, Ulinzi, Utawala, Kiuchumi, Kiteknolojia na Kijamii katika Idara ya Kilimo.

Mafanikio yaliyopatikana/fursa zilizopo;

- Katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru wakulima wamekuwa na uelewa mkubwa juu ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kupitia mashamba darasa na hivyo kufanya uzalishaji kuongezeka kwa 29% kwa mazao ya chakula na 54% kwa mazao ya biashara
- Pia wakulima wanatumia kilimo cha umwagiliaji ambapo jumla ya hekta 1,584 zinalimwagiliwa wilayani na hivyo kuongeza uzalishaji wa mpunga kutoka gunia 3 kwa ekari hadi gunia 33.5 kwa ekari.
- Aidha wakulima wamehamasishwa kutumia vikatuzi nguvu(Power tillers) katika kilimo ambapo kuna jumla ya vikatuzi nguvu 56 vilivyonunuliwa kupitia DADPS na kwa watu binafsi.Wilayani pia kuna jumla ya matrekta makubwa 48 ambayo yapo na yanafanyakazi. Vile vile wanyama kazi wameongezeka kutoka jozi 10 hadi jozi 74 mpaka sasa.
- Wakulima walinufaika na pembejeo za ruzuku kwa mazao ya chakula na vile vile ruzuku katika Korosho pia.
- Miradi mbali mbali imetekelezwa kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo Wilayani (DADPS) ambapo jumla ya vijiji 89 vimenufaika na program hii.

Changamoto zilizojitokeza:

- Uhaba wa wataalam wa kilimo/mifugo katika ngazi ya vijiji, hali hii husababisha wakulima kutopata huduma za ushauri wa kilimo ipasavyo.
- Bei kubwa ya pembejeo, hali inayofanya wakulima washindwe kununua pembejeo z kutosheleza mahitaji yao ya kilimo.
- Mwitikio mdogo wa wakulima katika kupokea elimu ya kilimo cha umwagiliaji kwa njia ya majaruba.

Matarajio ya taasisi katika miaka 50 ijayo:

- Matarajio ni kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kwa kutumia zana bora za kilimo na pembejeo bora.
- Ongezeko la wataalam wa ugani katika vijiji, angalau kila kijiji kiwe na mtaalam.
- Uhamasishaji wa matumizi ya zana za kilimo katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.